# KISWAHILI LUGHA

# DARASA LA TANO

# 2015

**AVAILABLE ONLINE AT:**

Schools Net Kenya Consultancy

**P.O. Box 8076 – 00200 Nairobi, Kenya | Tel: +254202319748**

**E-mail: infosnkenya@gmail.com | www.schoolsnetkenya.com**

**KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA**

**Muda: saa 1 dakika 40**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujaze nafasi 1 - 15 zilizoachwa wazi.***

Mwanafunzi kwa jina Rodah ni ___1___ anayesomea katika shule ___2___ msingi ___3___ Garissa. Anasoma katika ___4___ la tano. Mwanamwali ___5___ ni mpole, mtiifu na ___6___ tabia ___7___. Anapatana na kila mtu, wakubwa kwa wadogo, wazee hata ___8___. Tabia ___9___ nzuri zinafanya apendwe na walimu wake pamoja na wanafunzi wenzake. Licha ya kuwa na ___10___ ya kupendeza, yeye pia huongoza darasani kwa kazi yake ___11___. Kila wanapofanya mtihani ___12___ huibuka kuwa ___13___. Mara nyingi hutuzwa zawadi baada ya kila matokeo ya mtihani. Kama ___14___ walivyosema, "ukiviona ___15___ vimeundwa," mtoto huyu hapotezi wakati wake ovyo. Yeye na vitabu ni kama chanda na pete.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. mvulana | B. sichana | C. msichana | D. mwanagenzi |
| **2.** | A. za | B. cha | C. la | D. ya |
| **3.** | A. ya | B. wa | C. cha | D. kwa |
| **4.** | A. ndarasa | B. daraja | C. darasa | D. darasani |
| **5.** | A. huo | B. huyo | C. hicho | D. hiyo |
| **6.** | A. mwenye | B. mwenyewe | C. yenye | D. yenyewe |
| **7.** | A. kizuri | B. mzuri | C. zuri | D. nzuri |
| **8.** | A. wavulana | B. vijana | C. wake | D. wakongwe |
| **9.** | A. yake | B. chake | C. zake | D. pake |
| **10.** | A. matendo | B. maenendo | C. tabia | D. mara |
| **11.** | A. mzuri | B. zuri | C. nzuri | D. kizuri |
| **12.** | A. yeye | B. wewe | C. huo | D. mimi |
| **13.** | A. mzidi | B. mshindi | C. msindi | D. mshindi |
| **14.** | A. wagenda | B. washenga | C. wahenga | D. waenga |
| **15.** | A. vyalea | B. viaelea | C. vinaelea | D. vyaelea |

***Kuanzia swali la 16 - 30 jibu swali kulingana na maagizo uliyopewa***

**16.** Tumia kiulizi kifaacho.
Ni mwanagenzi ______ aliyepotea njia?
A. mgani
B gani
C. yapi
D. upi

**17.** Ni kiroboto ______ huumiza?
A. yupi
B. kipi
C. kigani
D. upi

**18.** Kamilisha methali:
Ushikwapo
A. tangaza usaidiwe
B. jitetee
C. shikana pia
D. shikamana

**19.** Nyanya yangu hapendi kwenda hospitali kwa sababu huogopa kudungwa
A. sindano B. shidano
C. shindano D. zindano

**20.** Andika kwa wingi na ukubwa.
Jani dogo limeanguka
A. Majani ndogo yataanguka
B. Majani madogo hayataanguka
C. Majani madogo yameanguka
D. Vijani vidogo vitaanguka

**21.** Neno jarida liko katika ngeli gani?
A. U - I B. I - ZI
C. Ki - vi D. Li - ya

**22.** Akisami $\frac{2}{7}$ huitwa?
A. Nusu saba
B. Subui mbili
C. Tusui mbili
D. Thumuni mbili

**23.** Mayai ______ baada ya kutagwa ili kuangua vifaranga.
A. huatamiwa
B. hukaliwa
C. huaguliwa
D. hulaliwa

**24.** Tegua kitendawili kifuatacho:
Niendapo hunifuata.
A. Kioo B. Kivuli
C. Kifuli D. Macho

**25.** Chagua kitenzi cha wingi wa:
"Wewe una afya njema".
A. Ninyi una afya njema
B. Wao wana afya njema
C. Nyinyi mna afya njema
D. Wao wana maafya mema

**26.** Shayiri hutumiwa kutengeneza
A. waili B. uji
C. kishendea D. pombe

**27.** Andika sentensi hii kwa lugha sanifu.
Samaki ile inaogelea sana
A. Samaki yule anaogolea sana
B. Masamaki wale wanaogelea sana
C. Samaki ule anaogeleanga sana
D. Samaki kile kinaogelea sana

**28.** Sentensi ifuatayo iko katika nafsi gani?
"Nyinyi mnakula nyama."
A. Nafsi ya kwanza umoja
B. Nafsi ya pili wingi
C. Nafsi ya kwanza wingi
D. Nafsi ya tatu wingi

**29.** Ugonjwa wa kufa ganzi unaotokana na kukatwa na vitu kama chuma, mawe au visiki huitwa
A. homa ya matumbo
B. kichocho
C. pepopunda
D. kifaduro

**30.** Mstari mmoja wa shairi huitwa
A. mshororo
B. kina
C. tarbia
D. ubeti

***Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali* 41- 50**

Edna Ganze
Shule ya Msingi ya Mbeo,
Meru - Kenya
Aprili 1, 2015

Kwa mpendwa Miriamu,

Kwanza pokea Salamu nyingi kama mchanga baharini kutoka kwa binamu yako.

U hali gani? Habari ya akina Esta? Je ushamwamisha shule ya bweni ya Bura na kumpeleka shule ya kutwa ya Mwembeni? Msalimie mjomba wangu bwana Emilio.

Kusudi la kukuandikia waraka huu ni kukujulisha kuwa wanafunzi wa darasa la nane wamepangiwa kuitembelea hifadhi ya mbuga ya wanyama ya Tsavo mashariki mnamo mwanzo wa Juni. Matembezi haya yana manufaa mengi sana licha ya kuwa raha, kwani tutaweza kusoma sana njiani na hata mbugani. Tutasoma jinsi wanyama wanavyokula, kutembea na hata kuwasiliana. Tutaweza kuziona sehemu kadha za nchi hii.

Jambo la <u>kunikera</u> ni kwamba mama yangu hawezi kumudu kunilipia shilingi elfu nne za shughuli hiyo. Pesa alizo nazo amepanga kumlipia dadangu mkuu karo na pesa ya mtihani wa kidato cha nne.

Nanyenyekea ni kikuuliza unilipie pesa hii ili nijiunge na wengine.Tumepewa mpaka tarehe 10 mei kuwa tumelipa pesa hiyo. Tafadhali nijibu pindi tu uipatapo barua hii.

Ni mimi wako Edna.

**41.** Barua ya anwani moja huitwaje?
A. Barua rasmi
B. Barua ya kikazi
C. Barua ya kindugu
D. Barua ya heshima

**42.** Ni sababu gani kuu katika barua hii iliyomfanya mwandishi aiandike?
A. Kusalimiana
B. Kusabahiana
C. Kuomba alipiwe pesa ya safari
D. Kuomba nafasi ya kwenda mbugani

**43.** Neno jingine la waraka ni
A. haraka
B. nyaraka
C. wa kwanza
D. barua

**44.** Dada yake mwandishi anaitwaje?
A. Raha
B. Ganze
C. Edna
D. Karo

**45.** Tsavo mashariki ni
A. hifadhi mbuga ya wanyama pori
B. sehemu ya Mombasa
C. dira
D. sehemu ya dunia

**46.** Miriamu ni nani?
A. Shangazi yake Ganze
B. Binamu yake ganze
C. Binamu yake karo
D. Hatujaambiwa

**47.** Esta katika ufahamu huu ni nani?
A. Dadake Edna
B. Dada yake Karo
C. Mtoto wake Mariamu
D. Mtoto wake Edna

**48.** Neno <u>kunikera</u> limepigiwa mstari kumaanisha
A. kushangaza
B. kunipendeza
C. kunifurahisha
D. kuniudhi

**49.** Ni kiwango gani cha elimu alicho nacho Karo?
A. Darasa la nne
B. Darasa la nane
C. Kidato cha nne
D. Hatujaelezwa

**50.** Mada ifaayo katika habari hii ni
A. Shule ya kutwa
B. Shule ya bweni
C. Kuomba usaidizi
D. Kuomba msamaha